# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS,**
**MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA**

## MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO

**SALAM ZA MWAKILISHI WA MWENYEKITI WA BODI YA WAKURUGENZI e-GA KWA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, MHE. GEORGE SIMBACHAWENE (MB), KATIKA UFUNGUZI WA KIKAO KAZI CHA NNE CHA SERIKALI MTANDAO (e-GA) FEBRUARI 06, 2024 KATIKA UKUMBI WA AICC ARUSHA.**

---

***Mhe. George Simbachawene (Mb);*** *Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,*

***Mhe. Dadi Horace Kolimba****; Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Arusha,*

***Ndug; Juma Mkomi****; Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.*

***Mha. Benedict Ndomba;*** *Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA),*

***Bw. Yusuf Hamad Rashid;*** *Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji Wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar (e-GAZ),*

***Wakurugenzi wa Halmashauri, Mashirika na Taasisi Mbalimbali,***

***Wakuu wa Idara za TEHAMA na Watumishi kutoka Taasisi mbalimbali,***

***Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, na Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao,***

***Waandishi wa Habari;***

***Mabibi na Mabwana;***

***Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,***

Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema na kuweza kukutana hapa leo, katika tukio hili muhimu la Kikao Kazi cha 4 cha Serikali Mtandao.

**Mhe. Waziri**, napenda kukushukuru kwa kuitikia wito wa kushiriki nasi katika kikao kazi hiki. Tunafahamu kuwa, unayo majukumu mengi na ya muhimu lakini ukaona ni vema ukajumuika nasi hapa leo. Ukiwa ndiye Waziri mwenye dhamana ya Serikali Mtandao ambaye kwetu sisi wewe ndiye mlezi wa Taasisi yetu, tunafarijika sana kuwa nawe hapa na tunakukaribisha sana.

Aidha, napenda kuwashukuru viongozi wote wa Serikali, Mashirika na Taasisi za Umma na binafsi, Watumishi kutoka Taasisi mbalimbali za Serikali, Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao na Waandishi wa Habari, kwa kukubali na kutenga muda wenu kuja hapa kushiriki nasi katika kikao kazi hiki.

**Mhe. Waziri,** Kikao Kazi hiki kinalenga kuwakutanisha wadau mbalimbali wa Serikali Mtandao, ili kutathmini hali ya utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao, kujadiliana kwa pamoja juu ya namna bora ya kukuza jitihada hizo, kuainisha changamoto zilizopo pamoja na kuazimia kuhusu njia za kukabiliana na changamoto hizo.

**Mhe. Waziri,** Mamlaka inatambua kuwa, ili kufikia dhamira ya Serikali ya utekelezaji wa jitihada za serikali mtandao kwa asilimia 100, Taasisi za Umma hazina budi kujiweka tayari kupokea na kutekeleza maelekezo utakayoyatoa hapa, ukiwa ndiye msimamzi mkuu wa serikali mtandao nchini. Maelekezo ambayo yanalenga kuzikumbusha taasisi za umma juu ya uzingatiaji wa Sheria ya Serikali Mtandao katika kuhakikisha matumizi sahihi na salama ya TEHAMA serikalini.

Aidha, Mamlaka inatambua na kuthamini ushirikiano na mchango mkubwa unaotolewa na wadau mbalimbali wa Serikali Mtandao, na kwa umuhimu huo Mamlaka imeandaa kikao kazi hiki ili kuendeleza ushirikiano huo kwa kujadiliana kwa pamoja namna bora ya kukuza jitihada za Serikali Mtandao nchini.

**Mhe. Waziri,** Mamlaka ipo tayari kupokea na kutekeleza maelekezo yako pamoja na maazimio yatokanayo na kikao kazi hiki kwa lengo la kuimarisha juhudi za Serikali Mtandao.

**Mhe. Waziri,** natamatisha salamu zangu kwa kuwashukuru nyote mliohudhuria hapa leo, kwani uwepo wenu ndio haswa unakamilisha tukio hili. K

**Mhe. Waziri,** naomba sasa nimkaribishe **Ndg. Juma Mkomi** Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ili aseme machache na kukukaribisha.

***Asanteni sana kwa kunisikiliza***